# Learning by Ear 2010 – Urban Exodus

## Episode 02: "Caught between exile and responsibility"

**Author: Alfred Dogbé**

**Editor: Yann Durand**

**Translator: Anne Thomas**

WAHUSIKA:

**Scene 1:**

- BEN ( UMRI WA MIAKA 29)
- BAKI (UMRI WA MIAKA 26)

**Scene 2:**

- BAKI (UMRI WA MIAKA 26)
- BEN
- ZEINA (UMRI WA MIAKA 24)

**Scene 3:**

- BAKI (UMRI WA MIAKA 26)
- ZEINA (UMRI WA MIAKA 24)
- BEN (UMRI WA MIAKA 29)

## Intro:

Karibu kwenye Learning by Ear, kipindi cha pili cha mfululizo wetu wa vipindi kuhusu uhamiaji mijini unaoitwa “Kukabiliana na wimbi la mabadiliko”. Tunafuatiliza masaibu ya vijana watatu walio na shahada za chuo kikuu wanaoamua kutafuta ajira nje ya mji.

Ben ana umri wa miaka 29 na ameacha kazi ya utumishi wa umma kuafikia ndoto yake ya kuutumia ujuzi wake kuwahudumia wanakijiji. Ameamua kurudi kijijini kuanzisha chama cha ushirika akishirikiana na marafiki zake wa tangu utotoni Zeina na Baki.

Zeina ni mwanauchumi na Baki ni mwanaelimujamii. Wanapendana. Tangu walipohitimu wamekuwa wakipata kazi za vibarua vya muda mfupi. Baki anajaribu juu chini kutimiza lengo lake la kuhamia nchini Marekani. Anatumai kwamba Zeina ataungana naye mara tu atakapopata kazi ya kudumu huko Marekani. Hata hivyo Zeina hadhani kwamba maisha ya ukimbizi ndilo suluhisho.

Katika kipindi hiki cha pili, tutashuhudia Zeina akimbembeleza Baki mpenzi wake ili asishirikiane na Ben kujaribu bahati yao kwenye mradi wake. Wote watatu wanaanza kuuzingatia mradi wenyewe:

## Scene 1: In town. Early afternoon at Café Hope.

**BEN, BAKI**

1. **ATMO: BAR ATMOSPHERE: DANCE MUSIC, SNIPPETS OF CONVERSATION, NOISE OF BOTTLES AND GLASSES**

2. **BEN (SHOUTING)** Baki! Baki!

3. **SFX: RAPID STEPS APPROACHING**

4. **SFX: HANDS CLAPPING**

5. **BAKI** Nimekuwa nikikutafuta mahali ambapo tumezoea kukaa kila mara.

6. **BEN** Tuko hapa mbali na vipaza sauti. Hapa tutapata kuelewana tunaposema.

7. **BAKI** Naam, kweli unayosema.

8. **SFX : NOISE OF A CHAIR BEING MOVED**

9. **BAKI** **(sighing)** ... Aaah, hatimaye!

10. **BEN** Mbona pumzi juu juu? Salama?

11. **BAKI** Mpiga picha ndiye ambaye amenichelewesha. Alitakikana kunipa picha mwendo wa saa moja unusu. Lakini amenikawisha mno. Imenibidi nipige mbio ili nisichelewe. Wala sijazipata picha zenyewe (**sighing**). Hata hivyo ameniahidi atanipa hizo picha baada ya nusu saa.

**12. BEN** Kwani ni picha za nini?

**13. BAKI** Ninashiriki kwenye bahati nasibu ya vibali vya kuhamia Marekani. Leo ndio tarehe ya mwisho iliyowekwa. Zeina yuko wapi?

**14. BEN** Nilifikiri mtaandamana.

**15. BAKI** Na yeye yumo. Kwani amechelewa wapi?

**16. BEN** Zeina hana mazoea ya kuvunja miadi. Je, umesoma taarifa ya mradi wangu? Una maoni gani?

**17. BAKI** Nisikize, sina muda. Inanibidi kwenda kuzichukua hizo picha kisha nirejee kwenye maskani ya mtandao kabla ya adhuhuri. Twende nyumbani kwa Zeina ili tusipoteze wakati.

**18. BEN** Sawa! Twende zetu!

**19. SFX: STEPS GOING AWAY**

**----- MUSIC -----**

**Scene 2: In town at Zeina's home.**

**ZEINA, BEN, BAKI.**

**20. ZEINA** Samahani. Ninaugua homa ya malaria. Natumai hamkuwa mkinisubiri.

**21. BAKI** Umepata dawa yoyote?

**22. ZEINA** Naam, siku mbili tu zijazo na nitapata nafuu, hata hivyo sina neno. Ben pita ukae!

**23. SFX: NOISE OF A CHAIR BEING MOVED**

**24. BEN** Asante.

**25. ZEINA** Naam, sasa tuko sote.

**26. BEN** Baki, natamani sana kupata maoni yako kuhusu mradi huu.

**27. ZEINA** Mimi pia.

**28. BAKI** Kusema kweli nimevutiwa sana na ujasiri wako. Kuandaa mradi kama huo na kuutekeleza katika nchi hii. Bila shaka hilo ni jambo linalohitaji ujasiri mkubwa!

**29. ZEINA** Huoni kama kwamba unaweza kutekelezeka?

**30. BAKI** Tukizingatia vikwazo vilivyopo hapa nchini…Utapata wapi uwezo wa kufanya lolote kwenye hali kama hii iliyojaa fujo?

**31. BEN** Kwani kuna jengine tuwezalo kulifanya katika hali hii?

**32. ZEINA** Kizazi chetu kina jambo moja tu la kuzingatia – kutekeleza mambo sisi wenyewe papa hapa nyumbani au tuandame njia ya wavivu ya kukimbilia nchi za kigeni.

**33. BAKI** Si uvivu unaowafanya watu kwenda kutafua riziki mahali pengine! Na wanaojidanganya punde hutambua kwamba ni njia ngumu na yenye vizingiti aina tofauti tofauti

**34. BEN** Ndiyo hivyo! Mimi niko tayari kulishughulikia kidhati jambo hili lakini nikiwa papa hapa nyumbani. Mimi mtu wa hapa hapa.

**35. BAKI** Umefafanua vilivyo, lakini taarifa ya mradi wa kibiashara inatakikana kuandaliwa kwa lugha nzuri wala si kwa lugha

ya kishairi.

**36. ZEINA** Vipi maudhui yake? Una maoni gani kuhusu maudhui yanayoshughulikiwa?

**37. BAKI** Ndiyo hayo ninayotaka kuyazungumzia sasa. Mpango wowote wa kibiashara unatakikana ueleze kinagaubaga baadhi ya mambo unayoshughulikia. Sivyo hali ilivyo.

**38. ZEINA** Kwani mradi wenyewe ni mbaya?

**39. BAKI** Tuchukulie kwamba tumo mkutanoni. Nitawauliza maswali kadha. Halafu nitaweza kutayarisha taarifa ya mradi…

**40. ZEINA** Hivyo ni kusema kwamba hutaki kujihusisha?

**41. BAKI** Nadhani tunahitaji kufanya mambo hivyo…

**42. SFX: PHONE RINGING**

**43. BAKI** (on the phone) Halo? … Sawa. Haya! … Naja sasa hivi.

(**to Zeina and Ben**) Nina jambo la dharura la kufanya.

**44. SFX: STEPS GOING AWAY**

**45. BAKI** (**going away**) Tukutane kwenye bustani karibu na maskani ya mtandao… hapo ni mahali patulivu… kiasi dakika 20?

**46. ZEINA** (**shouting**) Unakwenda wapi Baki?

(**to Ben**) Ana nini?

**47. BEN** (**evasively**) Eee… Sina hakika… sijui picha au nini. Yaache hayo, tuuwazie huu mradi huku tunapotembea.

**------- MUSIC ------**

**Scene 3: In the park**

**ZEINA, BEN, BAKI**

| | | |
|---|---|---|
| **48.** | **ATMO: Park. Calm atmosphere. Birds singing** | |
| **49.** | **ZEINA** | Ninaamini huu mradi utafaulu. Natumai tutafanikiwa kumshawishi… |
| **50.** | **BAKI** | (**from a distance**) Je, mko tayari? |
| **51.** | **BEN** | Aha umeshafika! Naam, tuanze. |
| **52.** | **BAKI** | **(sitting down on the grass)** Hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuongoza uchanganuzi wa mradi kuanzia mwanzo hadi mwisho… Je mradi huu unahusu nini? |
| **53.** | **BEN** | Kuna vigezo vitatu vya kutiliwa maanani. Kwanza, karibu vijana wote wa kijiji chetu walio na ujuzi wamo hapa mjini hawana kazi na hawajui hatma ya maisha yao ya siku za usoni. Wana ujuzi ambao haujatumiwa. Pili, nyumbani huko kijijini jamaa zetu wanakabiliana na hali kwa mitindo duni na rasilimali ndogo. Hatima yake ni umasikini na upungufu wa chakula. |
| **54.** | **ZEINA** | Wala hakuna mtu anayeshughulika kubadili hali ya mambo. |
| **55.** | **BEN** | Usiseme hivyo! Lakini ninakubali kwamba yote yanayofanywa hayajaleta mabadiliko ya maana. |
| **56.** | **BAKI** | Sawa. Hicho ndicho kiini cha mradi huu – hamasa zako lakini je, mradi wenyewe unahusu nini? Unataka kufanya |

nini?

**57.** **BEN** Ningependa kuanzisha chama cha ushirika cha kilimo kitakachojumuisha kundi la vijana waliohitimu vyuo vikuu ili tupate kutumia ujuzi wetu kuhudumia kijiji chetu.

**58.** **BAKI** Chama hicho kitafanya nini?

**59.** **BEN** Tutawapa wanakijiji huduma zetu ili wapate kutumia mbinu mwafaka, ambazo zitawanufaisha na ambazo zitakuwa bora kwa mazingira.

**60.** **BAKI** Nini matokeo ya mradi iwapo utatekelezwa kama mlivyopanga?

**61.** **BEN** Wanachama wa chama hicho watafanya kazi zao katika hali ya kuvutia itakayowanufaisha.

**62.** **ZEINA** Ukulima na uuzaji wa mazao ni bora. Hakutakuwa tena na upungufu wa vyakula. Hali ya maisha itkuwa nzuri.

**63.** **BEN** Hatua ya kuongeza shughuli za kilimo haitaathiri mazingira.

**64.** **ZEINA** Hali hiyo itawapa wakazi nafasi nzuri ya kupata haki zao za msingi za binadamu.

**65.** **BEN** Watu binafsi na jamii kwa jumla wataweza kustawi na kuwa na maisha mazuri.

**66.** **BAKI** Na vipi mnataraji kuafikia malengo hayo?

**67.** **ZEINA** Kwanza tunahitaji kupata wanaotuunga mkono.

**68. BEN** Nataraji wewe pia utahusika. Sisi watatu tuna ujuzi muhimu. Lakini sheria inasisitiza taratibu fulani kwanza zitimizwe. Tutahitaji kuwajumuisha watu wengi kwenye kundi letu.

**69. ZEINA** Lakini kwanza kabisa inatupasa kutayarisha mpango mwafaka wa kutekeleza mambo.

**70. BAKI** Mnataraji kutumia rasilimali gani?

**71. BEN** Tunahitaji ardhi, pembejeo na fedha. Lakini sijui kiasi gani?

**72. BAKI** Rasilimali mtaipata wapi?

**73. BEN** Tutapata!

**74. BAKI** Hilo si jibu mwafaka.

**75. ZEINA** Sidhani kwamba hilo swali linafaa.

**76. BAKI** Hakika?

**77. ZEINA** Ni wazo la mashirika fulani bandia yasiyo ya kiserikali, ambayo yanadumu kulangua fedha za wizi. Hapa hatuzingatii mtaji kabla ya mradi kuanzishwa lakini kinyume chake.

**78. BEN** Tutapata mtaji! Sijui kutoka wapi. Lakini ninajua jambo moja – mradi mzuri unaotunzwa na watu wenye ujuzi na ujasiri unaweza kuafikia lengo lake.

**79. ZEINA** Tuondokane na fikra hii ya watu wanaofaidi kutokana na miradi. Mitaji ni kiungo muhimu cha miradi yote ya maana.

| | | |
|---|---|---|
| **80.** | **BEN** | Tunahitaji kuungwa mkono na wanakijiji. |
| **81.** | **BAKI** | Kwa nini unadhani kwamba huenda ukatimiza malengo yako ya mradi huo katika siku za usoni? |
| **82.** | **BEN** | Tumebahatika kwa mambo mengi. Chama kitakuwa na wanachama wenye ujuzi na watakaojitolea kwa dhati. |
| **83.** | **ZEINA** | Chama kitakachozingatia taratibu za kisheria kina uzuri wake. Ni rahisi kukisimamia na hakina gharama nyingi. |
| **84.** | **BEN** | Na mfumo wake utaanza kufanya kazi mara moja. |
| **85.** | **ZEINA** | Vyama vya ushirika vimethibitika kuwa na ufanisi. |
| **86.** | **BAKI** | Sio kweli! Afrika, vyama vya ushirika vya kilimo havijafaulu. |
| **87.** | **ZEINA** | Baki! Unajua vizuri kwamba vyama hivyo vilianguka kwa kuwa vilianzishwa na serikali na si watu binafsi… Serikali haikukoma kuingilia masuala ya ndani ya vyama hivyo. |
| **88.** | **BEN** | Hatima yake ikawa hakuna demokrasia na pia wasimamizi hawakuwa na uhuru, ilhali hayo ndiyo masharti ya msingi kwa chama cha ushirika. Tutakuwa tunajihusisha moja kwa moja na malengo yetu. |
| **89.** | **ZEINA** | Nadhani wanakijiji watafurahia, na pia mashirika yanayoshughulikia wajasiriamali vijana, mashambani na mapambano dhidi ya umasikini. |
| **90.** | **BAKI** | Maana ya chama cha ushirika ni kundi la wataalamu wanaopendekeza huduma zao kwa wanakijiji. Je, walengwa |

wanahitaji huduma zilizopendekezwa?

**91. BEN** Bila shaka!

**92. BAKI** Pengine, lakini ninahitaji maelezo yaliyo bayana. Ikiwa wanaolengwa wanahitaji huduma hizo, inatakikana pia wawe na uwezo wa kuzigharamia. Je, wakulima wanaweza kulipia huduma hizo na je wenyewe wamekubali kugharamika? Je, gharama ni nafuu na inatia moyo kushughulika zaidi?

**93. BEN** Kwanza, hatutapata fedha nyingine, hilo tunalijua kwa uhakika. Lakini tutakuwa tukikinufaisha kijiji chetu. Manufaa hayo ni bora zaidi.

**94. BAKI** Kuna tatizo jingine. Nani atagharamia chama mwanzoni?

**95. BEN** Nimetundiza fedha kiasi.

**96. ZEINA** Mimi pia, ninaweza kuchangia.

**97. BAKI** Haya, sasa nitaandika taarifa ya mradi wa shughuli za chama. Hata hivyo itatubidi kwenda kijijini kutathmini iwapo mradi wenyewe unafaa na iwapo unaafikiana na hali halisi.

**98. ZEINA** Utaandamana nasi?

**99. BAKI** (**offended**) Kwani unanishuku kwamba siko tayari kusaidiana na marafiki zangu?

**100. BEN** Achana na hayo, tafadhali!

**101. BAKI** Mmenitwisha jukumu. Halijakamilika. Nimepanga nilishghulikie hadi mwisho wake. Pengine iwe hamridhii

mimi kulishughulikia!

**102. ZEINA** La Baki! Nafurahi unautumia muda wako kwenye mradi huu.

**103. BAKI** Sawa! Naomba kuondoka!… Inanibidi niondoke sasa.

**104. BEN** Bila shaka! Bila shaka! Asanta sana!

**105. BAKI** Zeina, nitarudi hivi punde!

**106. SFX: STEPS GOING AWAY RAPIDLY**

**107. ZEINA** Ben, unajua kinachomshughulisha? Kwa hisani yako niambie nini anachofanya!

**108. BEN** Anakwenda kwenye maskani ya mtandao. Anataka kushiriki kwenye bahati nasibu ya kibali cha kwenda kuishi Marekani.

**109. ZEINA** Na umemruhusu kuondoka?

**110. SFX: STEPS GOING AWAY**

**111. BEN** Zeina! Zeina…!

**Outro:**

Hivyo ndivyo makala ya *Learning by Ear* inavyokamilika hivi leo. Tunakushukuru kwa kusikiliza kipindi cha pili cha mfululizo wa "Kubaliana na Wimbi la Mabadiliko". Usikose kipindi kitakachofuata ili ujue jinsi wanakijiji wanavyouchukulia mradi wa Ben, Baki na Zeina.

Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutupatia maoni yako, fungua ukurasa wetu wa tovuti www.dw-world.de/lbe au utuandikie barua-pepe kupitia anwani lbe@dw-world.de.

Kumbuka kusikiliza kipindi kinachofuata!

**END OF EPISODE 2**